# Jinsi ya kukuza mtama

Mtama ni kundi la nyasi ndogo zenye mbegu zinazokuzwa ulimwenguni kote kama zao la nafaka kwa chakula cha binadamu na malisho ya mifugo.
Mtama huchukua jukumu muhimu katika kuzuia na kuponya maradhi kadhaa. Mtama una virutubishi vingi vilivyoboreshwa kiasili. Mtama ni chanzo kikubwa cha fumuele, madini kama vile magnesiamu, fosforasi, chuma, kalsiamu, zinki na potasiamu. Mtama huhitaji halijoto ya joto ili kuota na kukua vizuri na huathiriwa na baridi. Joto bora la udongo kwa ajili ya uotaji mzuri wa mbegu ni kati ya nyuzi joto 68 hadi 86.

## Mahitaji ya udongo

Mtama huzaa vizuri kwenye udongo tifutifu usiotuamisha maji. Mtama huenezwa na mbegu au nafaka.
Nitrojeni kwa kawaida ni kirutubisho muhimu zaidi katika uzalishaji wa mtama. Viwango vya nitrojeni vitakavyohitajika hutegemea mavuno, ukuaji wa mmea, pamoja na historia ya upandaji wa mazao. Nitrojeni nyingi sana kupita kiasi huathiri ukuaji wa mtama.

## Aina mbalimbali

Mtama huhitaji joto la wastani la angalau nyuzi joto 25 ili kutoa mavuno mengi katika mwaka husika. Wadudu na magonjwa si changamoto kubwa kwenye mtama lakini ndege ni tishio kuu.
Mtama aina ya pearl ni chanzo kikubwa cha fosforasi ambayo husaidia katika muundo wa seli za mwili. Mtama aina ya wimbi una kalsiamu na protini nyingi na kiwango kizuri cha madini ya chuma na madini mengine.

## Udhibiti wa wadudu

Panzi ni wadudu waharibifu zaidi kwenye mtama. Tumia dawa za kuua wadudu ili kudhibiti panzi. Viwavijeshi pia hushambulia mtama lakini bado vianaweza kudhibitiwa kwa njia ya kutumia dawa.
Mtama huwa tayari kuvunwa wakati mbeguzilizo kwenye sehemu ya juu ya gunzi zimekomaa. Mbegu zilizo katika sehemu chini ya

gunzi lazima iwe zimepoteza rangi yazo ya kijani kibichi. Kwa wakati huu, majani na mabua bado yainaweza kuwa rangi kijani kibichi.